HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO

TANGAZO LA ZABUNI ZA MAWAKALA WA KUKUSANYA USHURU,KAZI NA VIFAA/HUDUMA MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2017 – JUNI, 2018.

Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro inawatangazia wale wote wanaotaka kuomba zabuni za kukusanya ushuru,kazi na vifaa/huduma mbalimbali kwa kipindi cha Julai, 2017 mpaka Juni, 2018, wanakaribishwa kuomba zabuni hizo kama ifuatavyo hapo chini.

- JINA LA ZABUNI: FUNGU LA WAKALA WA KUKUSANYA VYANZO VYA MAPATO NAMBA YA ZABUNI: LGA/062/2017-2018/NC/01-52.

MASHARTI KWA WAOMBAJI WA UWAKALA WA KUKUSANYA USHURU KWA

KIPINDI CHA JULAI 2017-JUNI, 2018.

1. Kila mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania.

2. Wakala afanye utafiti na kuonyesha kiwango cha juu cha mapato atakayowasilisha Halmashauri.

3. Mwombaji awe na uwezo wa kukusanya Mapato kwa kutumia mfumo

wa kielektroniki (**Electronic Revenue Collection System)** na mafunzo juu

ya mfumo huo yatatolewa**.**

Mfumo wa kielektroniki unaotumika na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ni **"Local Government Revenue Collection Information System – LGRCIS".** Wakala atatakiwa kutumia Vifaa vya kukusanya Mapato **(Point of Sale- POS)** ambavyo vitakuwa vimeunganishwa na Mfumo wa ukusanyaji Mapato **(LGRCIS)** wa Halmashauri.

Wakala atatakiwa kuweka gharama za mtandao kwenye kifaa cha kupokelea mapato cha kielektroniki "**Point of Sale" (POS)** kwa kila mwezi ambazo si chini ya shilingi 15,000.00 kwa kila mwezi atakazotumia.

Usafi wa maeneo ya kazi ya ukusanyaji mapato ni juu ya wakala mwenyewe.

4. Mwombaji atakayepata Uwakala atatakiwa alipe amana ya miezi mitatu ya kiwango cha chanzo atakachopata, ambayo itaonyeshwa katika kabrasha la zabuni kwa kila chanzo. Fedha hizi atarudishiwa baada ya mkataba kuisha muda wake na endapo atakuwa hadaiwi.

5. Wakala atakayepata zabuni ya ukusanyaji mapato atakapotaka kujitoa baada ya kusaini mkataba,atapaswa kuilipa Halmashauri kiasi cha fedha sawa na miezi sita (6) ya kiasi alichokuwa anailipa Halmashauri kila mwezi baada ya kujitoa.

6. Ajira kwa wakusanya ushuru ni juu ya Wakala mwenyewe.

7. Stakabadhi zitakazotumika kukusanya ushuru zitapatikana Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro kwa kulipiwa na si vinginevyo na zitakuwa ni za mfumo wa kielektroniki.

8. Viwango vya kutoza ushuru ni vile vilivyopitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro kulingana na sheria ndogo.

9. Mwombaji asiwe Mheshimiwa Diwani, Mtumishi wa Halmashauri ya

Wilaya ya Simanjiro.

10. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya uwakala ya shilingi Tshs 100,000.00 (Laki moja tu) kwa kila chanzo na kupewa stakabadhi pamoja na kabrasha la zabuni ambalo atatakiwa

kulijaza na kulirudisha kabla ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ada ya maombi hairudishwi.

11. Mwombaji aambatanishe nyaraka zifuatazo:-

(i) Nakala ya Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN/VAT

Number)

(ii) Nakala ya leseni ya ukusanyaji Mapato hai

(iii) Nakala ya usajili wa Kampuni/Jina la Biashara.

(iv) Nakala ya stakabadhi ya ada ya maombi.

(v) Orodha ya wafanyakazi.

(vi) Orodha ya kazi za ukusanyaji mapato alizofanya kwa miaka (2) iliyopita; Ambatanisha nakala ya barua za uteuzi.

(vii) Mamlaka ya kisheria ya kukasimu madaraka (Power of attorney) kwa Makampuni

(viii) Endapo mwombaji ni mtu binafsi, sharti aonyeshe umiliki wa mali isiyohamishika na kama mwombaji hana hati miliki sharti Uthibitisho wa umiliki wa mali isiyohamishika uthibitishwe na vyombo vya kisheria.

(ix) Mwombaji aonyeshe uwezo wa kifedha wa kufanya kazi. Aambatanishe “Bank statement” ya kuanzia Julai 2016 hadi Januari 2017)

12. Maelezo mengine ambayo mwombaji anapaswa kuzingatia yanapatikana katika kabrasha la zabuni.

13. Maombi yafungwe katika bahasha kwa lakiri **(Seal)** na kuonesha namba ya Zabuni na aina ya sehemu anayoomba na kutumbukiza kwenye sanduku la zabuni lililopo katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Simanjiro

14. Maombi yaandikwe kwa:

MKURUGENZI MTENDAJI,

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO,

S. L. P 9596,

ORKESUMET-SIMANJIRO.

15. Waombaji wote mnakaribishwa kufika wenyewe au kutuma wawakilishi wenu siku ya ufunguzi. kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.

16. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **28-03-2017** saa tano (5:00) kamili asubuhi na Zabuni zitafunguliwa tarehe hiyo **28-03-2017** baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi, katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro uliopo makao makuu ya Wilaya Mjini Orkesumet.

17. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.

18. Maombi ambayo hayatazingatia masharti yaliyotajwa hapo juu

hayatafikiriwa.

19. Halmashauri hailazimishwi kwa njia yoyote kukubali ombi lolote.

- **2.** JINA LA ZABUNI: FUNGU LA UGAVI WA VIFAA NA HUDUMA MBALIMBALI**.**

NAMBA YA ZABUNI: LGA/062/2017-2018/NC/01-16.

MASHARTI KWA WAOMBAJI WA UGAVI WA VIFAA NA HUDUMA MBALIMBALI

Mwaombaji awe na leseni hai ya biashara

Awe amesajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kupata namba ya utambulisho (TIN).

Awe na utakaso (Tax clearance) kwa mwaka wa fedha uliopita

Mwombaji awe na ofisi na aonyeshe kwa maandishi mahali ilipo ofisi yake na zaidi itapendeza akiweka mchoro wa barabara ilipo ofisi yake.Aorodheshe bei ya vifaa/huduma ambazo ataiuzia Halmashauri.

Mwombaji aonyeshe jina la mmiliki au wamiliki wa biashara husika. (Certificate of registration or Articles and Memorandum of Association).

Madiwani na Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro hawaruhusiwi kuomba Zabuni.

Vitabu vya maelezo ya zabuni ambavyo vitauzwa na Halmashauri kwa wazabuni vifungwe kwa **LAKIRI baada ya kujazwa na wazabuni na** viwekwe kwenye bahasha za khaki zisizokuwa na alama yoyote ya kumtambulisha muombaji.

maelezo ya kila zabuni yanapatikana kwenye ofisi ya Kitengo cha Manunuzi kuanzia tarehe **15.03.2017,**baada ya muombaji kulipa ada ya **Tshs. 100,000 (Mia Moja Elfu tu)** kwa kila Zabuni atakayoomba na kupewa kitabu cha zabuni ambacho muombaji atalazimika kukijaza.Fedha za maombi hazitarudishwa.

mwisho wa kupokea barua za maombi ni **tarehe 28.03.2017 saa tano kamili asubuhi** na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.

Maombi yote yatumwe kwa:

MKURUGENZI MTENDAJI,

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO,

S.L.P. 9596,

ORKESUMET-SIMANJIRO.

-

-

- JINA LA ZABUNI: FUNGU LA ORODHA FUPI YA MAKANDARASI KWA AJILI YA KUFANYA KAZI ZA UJENZI,NAMBA YA ZABUNI: LGA/062/2017-2018/NC/

(Pre-Qualification of contractors For Civil and Building Works)

Awe na cheti/usajili hai wa Bodi ya Wakandarasi (CRB)

Awe na ofisi yenye mhudumu muda mwingi wa kazi na pia aonyeshe mahali ilipo ofisi yake (Mkoa, Wilaya, Mji, Mtaa na namba ya Nyumba)

Awe na TIN

Mwombaji wa Zabuni ya kazi za ujenzi ni lazima awe anatumia mashine ya kukusanya mapato ya Serikali (Electronic Fiscal Devices - EFDs).

Awasilishe orodha ya Wataalam wa Kampuni yake na sifa zao..

Aonyeshe orodha ya vifaa vya kazi anavyomiliki

Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili (2) na afungashe orodha ya miradi aliyowahi kufanya

Aonyeshe Bank statement za miezi mitatu ya Februari, Machi na Aprili 2013.

Madiwani na Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro hawaruhusiwi kuomba.

- Vitabu vya maelezo ya zabuni ambavyo vitauzwa na Halmashauri kwa wazabuni vifungwe kwa **LAKIRI baada ya kujazwa na wazabuni na** viwekwe kwenye bahasha za khaki zisizokuwa na alama yoyote ya kumtambulisha muombaji.
- Maelezo ya kila zabuni yanapatikana kwenye ofisi ya Kitengo cha Manunuzi kuanzia tarehe **15.03.2017,**baada ya muombaji kulipa ada ya **shilingi 100,000 (Mia Moja Elfu Hamsini tu)** kwa kila Zabuni atakayoomba ambazo hazitarudishwa.

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 28.03.2017 saa Tano kamili asubuhi** na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.

Maombi yote yatumwe kwa:

MKURUGENZI MTENDAJI,

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO

S.L.P. 9596,

ARUSHA.

Halmashauri hailazimishwi kwa njia yoyote kukubali ombi lolote.

NARCIS E.KISAKA,

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI (W),

SIMANJIRO.